



TIST HABARI MOTOMOTO AUGUST 2025

www.tist.org. Email: info@tist.org Tel. +255784-537720



In this newsletter, we are going to have;

- I. Identifying and Sharing Best Practices
- II. TIST Habari Moto Moto Newsletter
- III. TIST Best Practices “Kujengana”

Identifying and Sharing Best Practices

TIST encourages Small Groups to identify, adopt and share Best Practices appropriate for their local environment and circumstances. This comes from hands-on experience. Identification and sharing of Best Practices is a very powerful tool. It enables Small Group members to find out things that work from many other Small Groups around their country and the world.

Please identify and Share Best Practices about your tree nurseries, benefits of trees in your farm, bee keeping, fish keeping, livestock keeping and poultry, Conservation Farming, Leadership in your group, religious and political, businesses, environmental Best Practices like energy serving stoves etc. The first step in sharing Best Practices is to do so amongst your group members. You should discuss during weekly Small Group meetings any Best Practices identified by certain group members. If group members concur then Best Practices should be reported on Small Group Reports as well. Also when you meet members from other groups, tell them about the Best Practices identified by your group and ask them about any Best Practices they may have identified. You can share these Best Practices at your Cluster Meetings. You should also carefully take note of the Best Practices identified by other Small Groups and implement those in the operation of your groups in TIST activities.

TIST Habari Moto Moto Newsletter

The TIST Habari Moto Moto Newsletter is published every month. The newsletter covers news about TIST in your area and in other parts of the world. Newsletter includes many topics such as: information about Small Groups that have good results, what needs to be done about nurseries, tree planting, conservation farming and other sustainable development, announcements of upcoming events, reports on seminars and training, new and changed procedures, Best Practices identified by groups locally and worldwide, trends on how groups are performing. The newsletter is a very important source of information from TIST to the Small Groups and from Small Groups to other Small Groups locally and worldwide. Occasionally you may encounter a Cluster Servant or reporter working on developing articles for the Newsletter who may wish to interview and or photograph you and your planting sites.

In order to get information for publishing in the HMM, a publisher needs some information from farmers like you as individuals or as groups. The writer, Cluster Servant or group leader can arrange a meeting with you or your group members for an interview. Your voice notes, photos and/or videos may be taken to complete the relevant news or information. So we ask that before starting the interview please remind the interviewer to give you a consent form agreeing to have your information taken and allowing the information to be used by TIST.

TIST HABARI MOTO MOTO

Please give full cooperation and all efforts to enable the Project to get what is needed.

If your group has any ideas about a particular article that you would like to see published in the HMM, please give your suggestions to your group leader to submit a request to the writer or Cluster Servant for further action. Newsletters will be available every month and you should be able to pick them up from your monthly cluster meetings. Each Small Group will receive a copy of the newsletter. At least two group leaders should be present during the Cluster Meeting to collect the newsletter from the Cluster Servant on behalf of all your group members.



Photo: Farmers holding the HMMs during the Cluster Meeting

Kujengana: Don't miss the blessing for your Small Group

Kujengana is one of the Best Practices that TIST Small Groups identified and are practicing it. It is a very important part of your Small Group weekly meeting. It says in Ephesians 4:15- 16 that we are to build each other up into the fullness of Christ. Each person in your TIST Small Group brings his or her own special talents and gifts to the entire group. One of the wonderful things that happen in the Small Group is recognizing, sharing and using those God-given talents.

Kujengana is a way to let those talents be seen and be used. There are two parts to Kujengana:

Before the closing prayer, every person in the group says one specific, positive thing that the leader for that week did at that meeting. For example: he or she smiled when explaining things, kept to time, made good plans, encouraged all group members to speak, greeted me and made me feel welcome, pointed out something that was going very well in the meeting or in the work the group was doing, etc. Each member needs to say something different. This is not optional. Everyone gives Kujengana to the servant leader. Some groups also give Kujengana to the co-leader.

If someone sees a gift shown by the leader, a group member can also say that. With Rotating Leadership, each week a new leader will receive Kujengana. Through Kujengana, we encourage each other on the good things that week's leader did in the meeting and the talents the person showed.

Kujengana is also the way we learn to look for positive things about people and then say them. We all need to train our tongues to say the positive. In addition, the whole group learns what that group thinks is important in a servant leader. The next leaders will benefit from what they have heard in Kujengana about previous leaders and know what the groups think is important in being a servant leader.

In response to Kujengana, that week's servant leader just says, "thank you" after each group member's specific, positive statement. There is no discussion about how it could have been done better, or differently. Often, the person is happy when he or she is told the good things he or she did during the meeting. Sometimes we learn things about ourselves we didn't know! Kujengana helps the leader on that day recognize his or her talents and keeps on using them. Kujengana also helps the Small Group because all the members improve their servant leadership as they learn.

Kujengana is a double blessing!

TIST HABARI MOTO MOTO

TIST Values

As TIST Family we have our Values which most of TIST Small Groups know and practice. We always reflect on these Values and to ensure that we all are truly living by them. The success of TIST is based on the integrity and effort of individual members within TIST. What we can achieve depends on each of us following these Values;

Who are we?

- (i) We are Honest
- (ii) We are Accurate
- (iii) We are Transparent
- (iv) We are Servants to each other
- (v) We are Mutually Accountable to
Each Other and
- (vi) We create Low Budget/ cost, yet we
achieve Big Results

How we do things that other people can see

- 1) We are committed
- 2) We do our work in small groups
- 3) We seek and use the best way
- 4) We use our minds and hands.

What do we do?

- 1) We plant different species of trees for long -term
- 2) We find ways to improve our health
- 3) We practice Conservation Farming
- 4) We do other projects and businesses (sustainable
agriculture, nurseries, citrus growing, dairy goats and
farming, chickens, bee keeping, fishponds and fish
keeping, silkworm farming etc.)
- 5) We sell carbon credits

What do we create?

- 1) We create team work - by doing things this way;
we end up working as a team.
- 2) We create capacity - we create organization,
strength, and a system that is strong.
- 3) We create enjoyment - we see results, we
accomplish big things that we enjoy.
- 4) We create Big Results - In Conservation Farming
and from other projects and business that we do.
- 5) We create Big Results with Low Budgets



TIST HABARI MOTOMOTO AGOSTI 2025

www.tist.org. Email: info@tist.org Tel. +255784-537720



Katika jarida hili, tutakuwa na:

- (I) Kutambua na Kushirikishana Mbinu Bora
- (II) Jarida la TIST Habari Moto Moto
- (III) Mbinu Bora kwa njia ya “Kujengana”

TIST HABARI MOTO MOTO

Kutambua na Kushirikishana Mbinu Bora

Moja ya kanuni kuu za Mpango wa TIST ni kuviwezesha Vikundi Vidogo kutambua na kushirikishana Mbinu Bora zinazofaa kutumika kulingana na mazingira na uzoefu walionao katika mambo mbalimbali ili kufanikiwa kwenye Mradi. Mbinu Bora ni dhana yenye nguvu sana ambayo inawezesha wanavikundi kufahamu na kuzitumia hizo Mbinu Bora zilizofanya kazi na kufanikiwa kwenye vikundi vyao, kwenye vikundi vingine nchini mwao na ulimwenguni kote.

Tafadhali ainisha na utushirikishe Mbinu Bora ulizotumia na zikafanikiwa kuhusiana; uotes haji na utunzaji wa vitalu vya miti, utunzaji wa miti shambani mwako, ufugaji wa nyuki, ufugaji wa samaki, ufugaji wa wanyama mbalimbali na ndege, Kilimo Hifadhi, masuala ya Uongozi nani na nje ya kikundi chako, biashara, utunzaji wa mazingira kwa kutumia majiko banifu n.k.

Hatua ya kwanza ya kutushirikisha Mbinu Bora ni kuanza na zile zilizopo miongoni mweni wanakikundi. Wakati wa mikutano ya kila wiki ya Kikundi chenu mnapaswa kujadili Mbinu zote Bora zilizotambuliwa na wanakikundi chenu au kikundi kingine. Ikiwa wanachama ndani ya kikundi watakubaliana basi hizo Mbinu Bora zinapaswa kutolewa kwenye taarifa za Vikundi Vidogo. Pia mnapokutana na wanachama kutoka vikundi vingine, washirikishwe kuhusu Mbinu Bora zilizotambuliwa na kikundi chenu na wao washirikishe kuhusu Mbinu zao Bora ambazo wamezitambua na kuzitumia. Mnaweza kushirikishana Mbinu hizi Bora kwenye mikutano yenu ya Klasta.

Jarida la TIST Habari Moto Moto

Jarida la Habari Moto Moto huchapishwa kila mwezi. Kwa kawaida jarida hili linahusika na habari zinazohusu TIST katika eneo lako na maeneo mengine yanayotekeleza Mradi wa TIST. Linakuwa na mada nyingi kama vile: habari kuhusu Vikundi Vidogo ambavyo vina matokeo mazuri, nini kinahitajika kufanywa kuhusu vitalu, upandaji miti, kilimo hifadhi na maendeleo mengine endelevu, matangazo ya matukio yajayo, ripoti kuhusu semina na mafunzo, taratibu mpya na zilizobadilishwa, Mbinu Bora zinazotambuliwa na vikundi ndani ya nchi na ulimwenguni kote, mwelekeo wa jinsi vikundi vinavyofanya kazi. Jarida ni chanzo muhimu sana cha kushirikishana habari za TIST kwenda kwenye Vikundi Vidogo ndani ya nchi na ulimwenguni kote.

Ili kupata makala na taarifa za kuchapisha kwenye jarida; mara nyingi mwandishi wa HMM huhitaji taarifa kutoka kwa Wakulima kwa ajili ya wakulima au vikundi vingine kuweza kujifunza. Hivyo tunaomba taarifa zinapohitajika mwandishi wa Jarida la HMM au Mtumishi wa Klasta au Mwezes haji anaweza kukutana na Mkulima au wanavikundi kwa ajili ya mahojiano ili kupata taarifa sahihi zinazohitajika. Maelezo ya sauti yako, picha au video zinaweza kuchukuliwa ili kukamilisha habari au taarifa husika. Hivyo tunaomba kabla ya kuanza mahojiano tafadhali mkumbushe mchukua taarifa akupatie fomu ya ridhaa ya kukubali kuchukuliwa taarifa zako na kuruhusu taarifa hizo zitumike kwenye Mpango wa TIST.

TIST HABARI MOTO MOTO

Tafadhali toa ushirikino kikamilifu na jitihada zote ili kuwezesha Mradi kupata kile kinachohitajika. Ikiwa kikundi chako kina mawazo yoyote kuhusu makala Fulani ambayo ungependa kuona inachapishwa kwenye jarida, tafadhali toa mapendekezo hayo kwa Mwezeshaji wa kikundi chako ili awasilishe ombi kwa mwandishi na mawazo yako yatafanyiwa kazi.

Majarida ya HMM yanatolewa kila mwezi hivyo viongozi wa Kikundi chako wanapaswa kuhudhuria mikutano ya Klasta ya kila mwezi ili kupata nakala za jarida kwa niaba ya wanakikundi wote. Nakala za jarida zinachapishwa katika lugha mbili, ya Kiingereza na Kiswahili.



Picha: Wakulima wakiwa wameshikilia majarida Ya Habari Moto Moto baada ya mkutano wa Klasta

Kujengana: Usikose Baraka kwenye Kikundi chako Kidogo

Kujengana ni jambo la muhimu sana kufanyika kwenye mkutano wa kila wiki wa Kikundi Kidogo. Waefeso 4:15-16 Inasema kwamba tunapaswa kujengana katika utimilifu wa Kristo. Kila mtu katika Kikundi chake Kidogo cha TIST analeta talanta na vipaji vyake maalum kwa kikundi kizima. Moja ya mambo mazuri ya ajabu yanayotokea katika Kikundi Kidogo ni kutambua, kushiriki na kutumia talanta hizo tulizopewa na Mungu.

Kujengana ni njia ya kuruhusu vipaji hivyo kuonekana na kutumika. Kuna sehemu mbili za Kujengana:

- Kabla ya maombi ya kumaliza mkutano, kila mtu katika kikundi anasema jambo moja muhimu, chanya ambalo kiongozi wa juma hilo alifanya kwenye huo mkutano. Kwa mfano: alitabasamu, alitumia muda vizuri, alipanga mipango mizuri, alitia moyo wanakikundi wote kuzungumza, alisalimia na kumifanya nijisikie kuwa nimekaribishwa, alionyesha jambo ambalo lilikuwa likiendelea vizuri sana katika mkutano au katika kazi ambayo kikundi kilikuwa kikifanya, n.k. Kila mshiriki anahitaji kusema kitu tofauti. Jambo hili si hiari, kila mmoja anapaswa kumpa Kujengana Mwezeshaji wa wiki anayemaliza muda wake wa kutumika. Vikundi vingine pia vinatoa Kujengana kwa kiongozi mwenza.

- Ikiwa mtu anaona karama iliyoonyeshwa na kiongozi, mwanakikundi pia anaweza kusema kuhusu karama hiyo. Kwa Uongozi wa mzunguko, kila wiki kiongozi mpya atapokea Kujengana. Kupitia Kujengana, tunatiana moyo juu ya mambo mazuri ambayo kiongozi wa wiki alifanya katika mkutano na vipaji ambavyo mtu huyo alionyesha. Kujengana pia ni namna tunavyojifunza kuangalia mambo chanya kuhusu watu na kisha kuyasema. Sote tunahitaji kuzoeza ndimi zetu kusema mambo chanya. Aidha, Wanakikundi hujifunza kile ambacho kikundi hicho kinafikiri ni muhimu kwa kiongozi mtumishi. Viongozi watakaofuata watafaidika na yale waliyoyasikia katika Kujengana kuhusu viongozi waliopita na kujua nini Wanakikundi wanafikiri ni muhimu katika kuwa kiongozi mtumishi.

Kwa mujibu wa Kujengana, kiongozi mtumishi wa wiki hiyo anasema tu, "asante" baada ya kila mwanakikundi kutoa neno maalum na chanya. Hakuna mjadala kuhusu ambavyo wanakikundi wamekujenga namna ulivyofanya vizuri zaidi, au tofauti. Mara nyingi, mtu hufurahi anapoambiwa mambo mazuri aliyofanya wakati wa mikutano. Wakati mwingine tunajifunza mambo kuhusu sisi wenyewe tusiyoyajua! Kujengana humsaidia kiongozi siku hiyo kutambua vipaji vyake na kuendelea kuvitumia. Kujengana pia husaidia Kikundi Kidogo kwa sababu wanachama wote huboresha uongozi wao wa watumishi wanapojifunza.

Kujengana ni baraka tele!

TIST HABARI MOTO MOTO

MAADILI YA TIST

Kama Familia ya TIST tuna Maadili yetu ambayo wengi wa Wanavikundi Vidogo vya TIST wanayajua na kuyatekeleza. Daima tunatafakari juu ya Maadili haya na kuhakikisha kwamba sote tunaishi kulingana nayo. Mafanikio ya TIST yanatokana na uadilifu na juhudi za wanachama binafsi ndani ya TIST. Tunachoweza kufikia inategemea kila mmoja wetu kufuata Maadili haya;

Sisi ni Nani?

- 1) Sisi ni waaminifu.
- 2) Sisi tunatoa taarifa sahihi.
- 3) Sisi ni wawazi
- 4) Sisi tunatumikiana.
- 5) Sisi ni wawajibikaji
- 6) Bajeti Ndogo, Matokeo Makubwa

Jinsi tunavyofanya mambo ambayo watu wengine wanaweza kuona

- 1) Sisi tunajitolea.
- 2) Tunafanya kazi zetu katika vikundi vidogovidogo
- 3) Tunatafuta na kutumia njia bora
- 4) Tunatumia akili na mikono yetu.

Tunachofanya

- 1) Tunapanda aina mbalimbali za miti itakayodumu kwa muda mrefu.
- 2) Tunafanya mambo kuboresha afya zetu.
- 3) Tunafanya Kilimo Hai.
- 4) Tunafanya miradi na biashara zingine.
- 5) Tunafanya biashara ya hewa ya kaboni.

Tunafanya.

- 1) Tunaunda kazi ya timu—kwa kufanya mambo kwa njia hii; tunaishia kufanya kazi kama timu.
- 2) Tunajenga Uwezo-tunaunda shirika, nguvu, na mfumo ambao ni imara.
- 3) Tunafanya mambo yanayotufurahisha-tunaona matokeo, tunatimiza mambo makubwa ambayo tunafurahia
- 4) Tunafanya mambo yanayoleta matokeo makubwa-matokeo makubwa ya upandaji miti. matokeo makubwa katika Kilimo Hai na matokeo makubwa kutokana na miradi na biashara zingine tunazofanya.
- 5) Tunapata Matokeo Makubwa kwa kutumia Gharama Ndogo.